SEHEMU YA PILI

UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA BUNGE

Spika

3.-(1) Kutakuwa na Spika wa Bunge, ambaye atachaguliwa na atashika madaraka yake kufuatana na masharti ya Katiba na Kanuni hizi.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya Katiba na ya Kanuni hizi, wakati wowote ambapo Spika, kutokana na kutokuwepo nchini au maradhi au sababu nyingine yoyote, hataweza kutekeleza madaraka au majukumu ya kazi yake, basi madaraka na majukumu ya kazi yake yatatekelezwa na Naibu Spika.

Mamlaka ya Spika

4.-(1) Bila ya kuathiri masharti yanayofuatia Kanuni hii, Spika atakuwa ndiye Kiongozi wa Bunge, na ataliwakilisha Bunge katika vyombo na vikao vingine vyote nje ya Bunge.

(2) Spika ataongoza kila Kikao cha Bunge na ndiye mwenye mamlaka ya kuamua mambo yanayoweza kuzungumzwa Bungeni.

(3) Spika atawajibika kutilia nguvu Kanuni zote za Bunge, na endapo Mbunge yeyote hataridhika na uamuzi wa Spika anaweza kuwasilisha sababu za kutoridhika kwake kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni za Bunge ambayo itatakiwa ikutane mara moja kufikiria na kutoa uamuzi wake kwa Spika juu ya jambo hilo, na Spika atalijulisha Bunge uamuzi huo utiotolewa.

Isipokuwa kwamba Spika hatakuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni za Bunge wakati inapojadili jambo linaomhusu.

(4) Spika aweza kutamka Mbunge yeyote anayekiuka Kanuni hizi kujirekebisha mara moja, na Mbunge yeyote aweza kusimama mahali pake na kumwarifu Spika kuwa Mbunge fulani anakiuka kanuni kwa mujibu wa Kanuni ya 55(l),

(5) Spika aweza wakati wowote bila kutoa taarifa rasmi kwa Bunge,

kumtaka Naibu Spika au Mbunge ambaye ni Mwenyekiti wa Bunge kuongoza shughuli za Bunge.

Naibu Spika

5.-(1) Kutakuwa na Naibu Spika ambaye atachaguliwa na atashika madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba na Kanuni hizi.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya Katiba na ya Kanuni hizi, wakati wowote ambapo Spika na Naibu Spika wote hawapo au kwa sababu nyingine yoyote, hawawezi kutekeleza madaraka na majukumu yao, basi madaraka na majukumu hayo yatatekelezwa na Mbunge ambaye ni Mwenyekiti wa Bunge.

Mamlaka ya Naibu Spika

6.-(1) Naibu Spika atakuwa na Mamlaka na atatekeleza majukumu ambayo amepewa kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(2) Naibu Spika aweza wakati wowote anapokuwa amekalia Kiti cha Spika, bila kutoa taarifa rasmi kwa Bunge, kumtaka Mbunge ambaye ni Mwenyekiti wa Bunge kuongoza shughuli za Bunge.

Uchaguzi wa Spika

7.-(1) Kutakuwa na Uchaguzi wa Spika katika nyakati zilizowekwa na lbara ya 86(l) ya Katiba, na Uchaguzi huo utafanywa kwa kura ya siri kwa kufuata utaratibu uliowekwa na Kanuni hii.

(2) Kila Chama cha Siasa kitakuwa na haki ya kupendekeza jina moja, ama la Mbunge wa Chama hicho, au la mtu mwingine yeyote aliye na sifa za kuwa Mbunge, ambaye atakuwa mgombea uchaguzi wa Spika. Endapo jina moja tu ndilo litakuwa limependekezwa,basi mgombea huyo atahesabiwa kuwa anaungwa mkono na Vyama vyote vilivyowakilishwa, Bungeni, kwa hiyo atatangazwa kuwa amechaguliwa kuwa Spika bila kupingwa.

(3) Endapo wamependekezwa wagombea wawili au zaidi, uchaguzi utafanyika kwa kufuata utaratibu unaoelezwa katika fasili zinazofuata za Kanuni hii.

(4) Kabla ya kikao cha Bunge cha kumchagua Spika, Katibu ataandaa karatasi za kura zitakazoonyesha majina ya wagombea wote waliopendekezwa kwa mujibu wa fasili ya (2) ya Kanuni hii, na atatoa karatasi moja tu ya kura kwa kila Mbunge wakati wa kupiga kura.

Isipokuwa kwamba Mbunge ambaye kabla ya shughuli za uchaguzi

kumalizika atakosea katika kuweka alama kwenye karatasi ya kura ataruhusiwa kumrudishia Katibu karatasi hiyo naye Katibu ataifuta na kuiharibu mara moja na kumpa Mbunge huyo karatasi nyingine.

(5) Kila Mbunge atapiga kura kwa kuweka katika karatasi aliyopewa na Katibu alama ya "V" katika mraba pembeni mwa jina la mgombea anayemtaka awe Spika, na ataitumbukiza katika sanduku la kura.

(6) Baada ya Katibu kuridhika kwamba Wabunge wote waliomo Bungeni wanaotaka kupiga kura wameweka karatasi zao za kura katika masanduku, masanduku yote yatapelekwa mahali palipoandaliwa kwa kazi ya kuhesabu kura, na kura hizo zitahesabiwa chini ya usimamizi wa Wabunge watakaoteuliwa, mmoja mmoja kutoka katika kila chama kilichoshiriki katika uchaguzi huo.

(7) Mgombea yeyote wa kiti cha Spika atatangazwa kuwa amechaguliwa kuwa Spika iwapo atapata kura nyingi zaidi kuliko mgombea mwingine yeyote.

(8) Mara baada ya Katibu kumtangaza mgombea aliyeshinda Uchaguzi kwa mujibu wa Kanuni hii, Spika aliyechaguliwa ataapishwa kwa mujibu wa utaratibu wa Kanuni ya 25(2).

(9) Mgombea yeyote anaweza kumtaarifu Katibu kwa maandishi kwamba anajitoa kugombea, kabla ya shughuli za kupiga kura kuanza Bungeni, na Katibu atalifuta jina la mgombea huyo katika karatasi za kura.

Uchaguzi wa Naibu Spika

8.-(1) Kutakuwa na Naibu Spika wa Bunge ambaye atachaguliwa kutoka miongoni mwa Wabunge.

(2) Uchaguzi wa Naibu Spika utafanyika katika Mkutano wa Kwanza wa Bunge jipya, au mapema iwezekanavyo baada ya wakati huo; au katika kikao cha kwanza cha Bunge mara baada ya nafasi ya Naibu Spika kuwa wazi, au mapema iwezekanavyo baada ya kikao hicho.

(3) Uchaguzi wa Naibu Spika utaendeshwa kwa utaratibu ule ule

unaotumika kumchagua Spika, isipokuwa kwamba Mbunge hawezi kushiriki katika Uchaguzi wa Naibu Spika iwapo hajaapa Kiapo cha Uaminifu.

Uchaguzi wa Wenyeviti wa Bunge

9.-(1) Kutakuwa na Wenyeviti wawili wa Bunge ambao watachaguliwa na Wabunge kutoka miongoni mwa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge.

(2) Uchaguzi wa Wenyeviti wa Bunge utafanyika kwa kufuata utaratibu kwamba karatasi ya kura itakuwa na majina ya Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu. Kila Mbunge atapiga kura ya kuchagua majina mawili katika orodha hiyo. Wagombea wawili watakaokuwa wamepata kura nyingi zaidi kuliko wenzao, ndio watakuwa, wamechaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge,

9A. Uchaguzi wa Wabunge wanaokwenda katika vyombo vingine ambavyo kwa mujibu wa sheria zilizounda vyombo hivyo vinatakiwa viwe na wawakilishi wa Bunge, na uchaguzi unaofanywa na Bunge wa kuchagua Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki, utafanywa kwa kuzingatia, kura kadri iwezekanavyo, uwiano wa idadi ya Wabunge wa vyama mbalimbali vya siasa vinavyowakilishwa Bungeni, uwakilishi wa jinsia, na uwakilishi wa pande zote mbili za Muungano.

Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni

10. Waziri Mkuu atakuwa ndiye Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. Kama Waziri Mkuu hataweza kuwepo Bungeni kwa kipindi kinachozidi siku moja, atamteua Waziri mwingine kuwa Kiongozi wa muda wa Shughuli za Serikali Bungeni. Katika kufanya uteuzi huo, Waziri Mkuu atazingatia ukubwa kazini wa Mawaziri waliopo.

Kiongozi wa Upinzani Bungeni

11.-(1) Kiongozi wa Upinzani Bungeni atachaguliwa kwa kufuata utaratibu ulioelezwa katika fasili za Kanuni hizi zinazofuata.

(2) Chama chochote hakitakuwa na haki ya kuchagua Kiongozi wa Upinzani Bungeni, mpaka kiwe kina idadi ya Wabunge wasiopungua thelathini.

(3) Endapo kutakuwa na Vyama zaidi ya kimoja ambavyo kila kimoja kina Wabunge thelathini au zaidi, basi Chama chenye idadi kubwa zaidi ya Wabunge kuliko vingine ndicho kitakuwa na haki ya kuchagua Kiongozi

wa Upinzani Bungeni. Lakini endapo kutakuwa na vyama viwili au zaidi vyenye idadi sawa ya Wabunge ambao ni zaidi ya thelathini, Wabunge wa Vyama hivyo vinavyohusika watachagua Kiongozi wa Upinzani Bungeni kwa kufuata utaratibu watakaokubaliana wenyewe. Isipokuwa kwamba Vyama zaidi ya kimoja vikikubaliani kushirikiana katika shughuli za Upinzani Bungeni, na ushirikiano huo ukiunganisha Wabunge zaidi ya thelathini, na pia ikiwa idadi hiyo itakuwa kubwa zaidi kuliko Wabunge wa Chama kingine chochote cha upinzani basi vyama hivyo vilivyoshirikiana vitakuwa na haki ya kuchagua Kiongozi wa Upinzani Bungeni.

(4) Iwapo Wabunge wote wa Vyama vya Upinzani waliopo Bungeni watakubaliana kushirikiana katika shughuli za Upinzani Bungeni, basi watakuwa na haki ya kuchagua Kiongozi wa Upinzani, hata kama idadi yao haifikii Wabunge thelathini, lakini haipungui ishirini.

Naibu Kiongozi wa Upinzani na Wasemaji Wakuu Bungeni

12.-(1) Chama chenye haki ya kumchagua Kiongozi wa Upinzani Bungeni kwa mujibu wa fasili ya (3) ya Kanuni ya 11, chaweza pia kuchagua Naibu Kiongozi wa Upinzani.

(2) Kiongozi wa Upinzani Bungeni anaweza kuteua Mbunge wa Chama chake au wa Kambi yake ambaye atakuwa ndiye Msemaji Mkuu kwa kila Wizara iliyopo ya Serikali.

Waratibu wa Vyama Bungeni

13.-(1) Chama kinachounda Serikali na Chama chenye haki ya kuchagua Kiongozi wa Upinzani Bungeni, vyaweza kuteua Waratibu wa Vyama hivyo Bungeni, ambao watajulikana kwa jina la *"Chief Whip "* wa Serikali na *"Chief Whip* " wa Upinzani, Vyama hivyo vyaweza pia kuchagua Waratibu Wasaidizi ambao watajulikana kwa jina la (whips) *"Assistant whips"* Idadi hiyo itaamuliwa na Vyama vyenyewe.

(2) Kazi ya Viongozi hawa, kwa upande wa Serikali ni kuwa kiungo cha mawasiliano baina ya Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, na Wabunge wa Upande wa Serikali; na kwa upande wa Upinzani, pia ni kuwa kiungo cha mawasiliano baina ya Kiongozi wa Upinzani Bungeni, na Wabunge wa Upinzani.

(3) Kwa madhumuni ya Kanuni hii "Chama" maana yake ni Kamati za Vyama vya Siasa zilizotajwa katika Kanuni ya 83A ya Kanuni hizi.

14.-(1) Kutakuwa na Katibu wa Bunge ambaye atawajibika kuliakikisha

Katibu wa Bunge

utekelezaji bora wa Shughuli za Bunge kwa madhumuni hayo:-

(a) atahudhuria vikao vyote vya Bunge na vya Kamati ya Bunge Zima na, kama akiagizwa hivyo na Spika, vikao vya Kamati nyingine yoyote ya Bunge;

(b) atawajibika kuweka kumbukumbu zinazotakiwa ziwekwe kwa mujibu wa Kanuni hizi;

(c) atatayarisha Taarifa Rasmi, kwa mujibu wa Kanuni hizi;

(d) atatayarisha siku hadi siku Kitabu cha Shughuli za Bunge na kukihifadhi Ofisini kwake, kikiwa kinaonyesha:-

(i) maagizo yote yaliyotolewa na Bunge;

(ii) shughuli zote zilizopangwa kufanywa siku yoyote ya baadaye;

(iii) taarifa zote za maswali na hoja zilizokubaliwa na Spika.

(2) Katibu atawajibika kuhakikisha utunzaji mzuri wa kumbukumbu za Bunge, Miswada na Hati nyingine zilizowasilishwa Bungeni, na Mbunge yeyote aweza kukagua kumbukumbu na Hati hizo wakati wowote unaofaa; na vile vile watu wengine waweza kuzikagua, kwa kufuata utaratibu utakaowekwa na Spika.

(3) Katibu atawajibika kutunza na kuweka Kitabu cha Maamuzi ambamo ataingiza mara kwa mara kumbukumbu za maamuzi ya Spika kuhusu masuala ya utaratibu Bungeni.

(4) Katibu atawajibika kuhakikisha kuwa Ukumbi wa Mikutano na mazingira yake, huduma kwa Wabunge na vifaa vingine vinavyohusika na shughuli za Bunge, viko katika hali inayofaa kuliwezesha Bunge kutekeleza wajibu wake ipasavyo.

Ofisi ya Bunge

15.-(l) Bila ya kuathiri Masharti ya Katiba na ya Kanuni hizi kuhusu uwekaji wa nafasi na ngazi za utumishi katika Ofisi ya Bunge, Ofisi hiyo itagawanyika katika Idara, Sehemu na Vitengo mbalimbali kwa namna na idadi itakayoiwezesha kutoa huduma kamilifu kwa Wabunge, Bunge na Kamati zake mbalimbali.

(2) Katibu atawajibika kuhakikisha kwamba Ofisi ya Bunge inaandaa

shughuli na kutoa huduma nyinginezo kwa Wabunge, Bunge na Kamati zake kwa kuzingatia utaratibu utakaoagizwa na Spika au utakaowekwa na Bunge au Kamati inayohusika.

(3) Bila ya kuathiri masharti yaliyotangulia ya Kanuni hii, kutakuwa na Makatibu Wasaidizi wa Bunge kwa idadi na ngazi mbalimbali kadri itakavyoamuliwa na Tume ya Huduma za Bunge iliyoundwa kwa mujibu wa Sheria Na. 14 ya 1997. Watumishi wa Bunge

(4) Kutakuwepo na watumishi wengine wa Bunge ambao nyadhifa, kazi na idadi yao vitaamuliwa na mamlaka inayohusika.

16. Kutakuwepo na Mpambe wa Bunge ambaye atatekeleza shughuli mbalimbali za Spika na za Bunge kwa kufuata maagizo atakayopewa na Spika au na Katibu, kadri itakavyokuwa. Mpambe wa Bunge

17.-(1) Pamoja na kutekeleza shughuli mbalimbali kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 16, Mpambe wa Bunge:- Majukumu ya Mpambe wa Bunge

(a) atamtangulia Spika, akiwa amebeba Siwa ya Bunge, wakati Spika anapoingia na anapotoka kwenye Ukumbi wa Mikutano ya Bunge, kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa;

(b) atahakikisha utulivu na amani katika sehemu wanapokaa wageni na atawawekea utaratibu maalum wa kuingia na kutoka Bungeni;

(c) atasimamia masuala yote ya ulinzi na usalama wa Ofisi na majengo yote ya Bunge, ikiwa ni pamoja na mali na vifaa vya Bunge.

(2) Kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa majukumu yake wakati wa vikao vya Bunge, Mpambe wa Bunge aweza kutoa maagizo anayoona yanastahili kutolewa kwa Wahudumu wa Bunge, na watumishi hao watawajibika kutekeleza maagizo hayo.

(3)Mpambe wa Bunge atawajibika kuratibu na kushauri juu ya usalama wa Ukumbi, majengo na vyumba vyote vya Bunge na pia sehemu zote za majengo yote yanayotumiwa na Bunge au Kamati za Bunge.

(4) Mpambe wa Bunge atakuwa na uwezo wa kutoa maagizo kwa Askari Polisi au Askari mwingine yeyote aliyekabidhiwa kazi katika Ukumbi wa Bunge na mazingira yake au katika majengo, vyumba au sehemu nyinginezo zinazotumiwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za Bunge kwa mujibu wa Kanuni hizi.